

**BURLANI RAIS DKT. JOHN MAGUFULI -1959-2021**  
**MIAKA 6 YA HAYATI RAIS MAGUFULI**



# Wakazi Kilimanjaro watakiwa kumuenzi JPM kwa kuanzisha kiwanda cha ngozi

NA JACKSON KIMAMBO,  
MOSHI

WAKAZI wa Mkoa wa Kilimanjaro wametakiwa kumpongeza na kumuenzi Hayati Dkt. John Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa uzalendo na upendo wake wa kuanzisha kiwanda cha kimataifa cha ngozi Kilimanjaro kilichopo Mjini Moshi.

Afisa habari na masoko wa kiwanda cha kimataifa cha ngozi Kilimanjaro (Kilimanjaro international leather industry manufacturing) Fredrick Njoka aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kiwanda hicho na kutoa wito kwa wananchi kupenda kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Alisema utekelezaji wa ujenzi wa kiwanda hicho ni ndoto zilizoanzishwa na Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere



toka mwaka 1977 alipoanzisha kiwanda cha kutengeneza viatu vya kijeshi.

Njoka alisema katika kukuza uchumi wa Taifa la Viwanda Hayati Dkt. Magufuli alitilia mkazo kuhakikisha uzalishaji unaongezeka na kiwanda hicho kimekuwa kikipanuka zaidi ili kiweze kukidhi mahitaji ya soko kitaifa na

kimataifa.

Alisema Tanzania ni nchi ya pili barani Afrika ikitanguliwa na Ethiopia kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo na kwamba lengo la kuanzishwa kwa kiwanda hicho hapa nchini ni kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa ngozi.

Njoka alisema kiwanda

hicho tayari kimefungua milango kwa wafugaji kuuzua ngozi kiwanda cha Kilimanjaro ili liweze kuongeza thamani ya mnyororo kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwa kutumia ngozi.

Alisema uwekezaji uliofanyika katika kiwanda hicho ni mkubwa na umega-wanyika katika sehemu

nne ikiwemo kiwanda cha kuchakata ngozi ambapo pia kitahusika na kuzalisha mali ghari za kulisha viwanda vingine.

Sehemu nyingine ni kiwanda cha kutengeneza soli na sehemu ya kuhifadhi mali ghafi ndani ya kiwanda na kwamba asilimia 60 ya bidhaa zinazozalishwa zitauzwa hapa nchini na asilimia 40 zitauzwa kimataifa.

Njoka alisema kukamilika kwa kiwanda hicho ni faraja kubwa kwa wafugaji na Watanzani kwa ujumla kwani kiwanda hicho kitanunua ngozi za wafugaji hapa nchini kutoa ajira zaidi ya watu 3,000 na kuchangia pato la Taifa.

Alitoa wito kwa wananchi kupenda kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwa lengo la kuchochea ukuzaji wa pato la Taifa kwani kuwapo kwa kiwanda cha viatu na bidhaa za ngozi ni fahari kwa Kilimanjaro uchumi unaanza kuinuka.





## Watanzania watakiwa kumuenzi Hayati Dk. Magufuli kwa uzalendo

NA MWANDISHI WETU

**W**atanzania wametakiwa kumpongeza na kumuenzi Rais wa zamani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli kwa uzalendo na upendo wake wa kuanzisha kiwanda cha Kimataifa cha ngozi Kilimanjaro kilichopo Mjini Moshi.

Afisa Habari na Masoko wa kiwanda cha ngozi Kilimanjaro, Fredrick Njoka, ameyasema hayo wakati alipokuwa akizungumza na Waandishi wa Habari waliotembelea kiwanda hicho na kutoa wito kwa wananchi kupenda kununua na kutumia bid-

haa zinazozalishwa hapa nchini.

Amesema utekelezaji wa ujenzi wa kiwanda hicho ni ndoto za zilizoanzishwa na hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere tangu mwaka 1977 alipoanzisha kiwanda cha kutengeneza viatu vya jeshi.

Njoka amesema katika kukuza uchumi wa Tanzania ya Viwanda, Hayati Dk. Magufuli alitilia mkazo kuhakikisha uzalishaji unaongezeka na kiwanda hicho kimekuwa kikipanuka zaidi ili liweze kukithi mahitaji ya soko Kitaifa na Kimataifa.

Amesema Tanzania ni Nchi ya pili barani Afrika ikitanguliwa na Ethiopia kwa kuwa na idadi kub-

wa ya mifugo na kwamba lengo la kuanzishwa kwa kiwanda hicho hapa nchini ni kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa ngozi.

Njoka amesema kiwanda hicho tayari kimefungua milango kwa wafugaji kuza ngozi kiwanda cha Kilimanjaro ili liweze kuongeza thamani ya mnyororo kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwa kutumia ngozi.

Amesema uwekezaji uliofanyika katika kiwanda hicho ni mkubwa na umegawanyika katika sehemu nne ikiwemo kiwanda cha kuchakata ngozi ambapo pia kitahusika na kuzalisha malighafi za kulisha viwanda vingine.

Sehemu nyingine ni kiwanda cha kutengeneza soli na sehemu ya kuhifadhi mali ghafi ndani ya kiwanda na kwamba asilimia 60 ya bidhaa zinazozalishwa zitauzwa hapa nchini na asilimia 40 itauzwa kimataifa.

"Kukamilika kwa kiwanda hicho ni faraja kubwa kwa wafugaji na Watanzani kwa ujumla kwani kiwanda hicho kitanunua ngozi za wafugaji hapa nchini kutoa ajira zaidi ya watu 3,000 na kuchangia pato la taifa.

"Nitoe wito kwa wananchi kupenda kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwa lengo la kuchochea ukuzaji wa pato la Taifa," amesema Njoka.